**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, BIASHARA NA UTALII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwezesha kuwa na afya njema na kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu katika kutekeleza majukumu ya kulijenga taifa letu. Pia, nachukua nafasi hii adhimu kwa moyo wa dhati kabisa, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kutoa maoni ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nichukue nafasi hii niwashukuru watendaji Wizara ya Biashara ambayo inaongozwa na Mheshimiwa **Omar Said Shaaban** kijana ambae tunaamini kwa kushirikiana na watendaji wa Wizara hiyo, maendeleo katika sekta ya viwanda na biashara yatapatikana kama inavyoelekezwa katika mipango na melekezo ya Serikali pamoja na ilani ya uchaguzi ya **Chama cha Mapinduzi.** Sisi Kamati tuna imani sana na utendaji na kipawa cha Mheshimiwa Waziri katika utendaji wake, lakini kama tunavyojua ***"Kipawa chochote cha mtu kama hakikuongozwa vyema huweza kuwa hatari au maangamizi kwa wengine"***, hayo ni maneno ya Mwandishi mahiri kabisa barani Afrika **Shaaban Robert** aliyoyasema katika Riwaya yake ya **Kusadikika**. Hivyo, pamoja na kipawa na ueledi wa Mheshimiwa Waziri tunamuomba asiache kuifuata miongozo iliyowekwa ili jahazi letu katika sekta hizi liweze kufika pale tunapopataka.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii inajumuisha Wajumbe wa aina tofauti ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa ni chachu ya kazi nzuri tunayoendelea kuifanya ndani ya Kamati hii. Naomba nichukue nafasi hii kwa heshima kubwa kabisa niwatambue Wajumbe hao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ali Suleiman Ameir | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Azza Januari Joseph | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Ali Abdulgulam Hussein | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mwanajuma Kassim Makame | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Nassor Salim Ali | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Said Saleh Salim | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Aziza Waziri Kheir | Katibu |
| 9. | Ndg. Mwaka Mwinyi Waziri | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,** Kuikuza na kuinyanyua sekta ya biashara na viwanda kunahitaji umakini mkubwa sana hasa tukizingatia kwamba sekta hizi mbili zinahitaji utayari na mafunzo mengi ambayo yatawasaidia wahusika kutekeleza malengo waliyojipangia kupitia ujuzi walioupata katika mafunzo waliyopatiwa awali. Ikumbukwe kwamba Serikali ya awamu ya nane imejidhatiti kabisa katika suala zima la uchumi wa buluu jambo ambalo ukuaji wake kwa kiasi kikubwa unategemea pia sekta ya biashara na viwanda, kama tunavyojua sekta ya viwanda ni sehemu muhimu ya uchumi wa kisasa ambao ukuaji na uimarikaji wake utaisaidia sana Serikali kutimiza ahadi zake kwa wananchi wake. Ili kuyafika hayo bajeti ya kutosha katika sekta hizi mbili inahitajika kutokana na unyeti wake.

**Mheshimiwa Spika**, katika hotuba yake ya uzinduzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alieleza kwa uwazi kabisa azma yake ya kufanya mapinduzi ya kiuchumi ambayo yana lengo la kuiondoa Zanzibar ilipo hivi sasa na kuipeleka mbele kwa kuikuza sekta ya viwanda,uvuvi, ufugaji, ukulima wa mwani, uchimbaji wa mafuta na gesi pamoja na kuweka matumizi sahihi ya rasilimali mbali mbali zilizopo baharini. Mambo yote hayo yanategemeana huku sekta ya viwanda na biashara ikichukua nafasi kubwa katika kuyaendeleza hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu ilipitisha bajeti ya Wizara ya Bisahara na Maendeleo ya Viwanda kwa kuangalia ahadi za Mheshimiwa Rais katika kampeni zake katika sekta hizi pamoja na malengo yake kama nilivyonukuu kidogo katika hotuba yake aliyokuja kuiwasilisha hapa Barazani wakati wa uzinduzi wa Baraza hili.

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuanza kuelezea Programu kuu na ndogo za Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022 naomba kwanza nichukue fursa hii kuelezea maoni ya Kamati kuhusiana na mapato ya Wizara kwa mwaka wa 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kilimo Biashara na Utalii, ilipitia mafungu ya mapato ya Wizara hii na kubaini kuwa kuna baadhi ya mafungu ya mapato yamechanganywa. Hivyo, Kamati inashauri mafungu hayo kwa mwaka ujao yatolewe maelezo ya kina na Wizara na waeleze iwapo katika mafungu hayo wapi kuna faida na wapi kuna hasara. Pia Kamati imeona kuna baadhi ya maeneo ya kibiashara yanakodishwa na Wizara bila kutoa maelezo ya kina kuhusiana na mapato hayo. Hivyo Kamati inaishauri Wizara kwa mwaka ujao mapato yanayopatikana kutokana na ukodishaji huo yaainishe kwa uwazi mapato ya Pemba ni yepi na mapato ya Unguja yepi.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na maelezo yaliyotolewa kwa Kamati, ilibainika kuwa mapato yanayokusanywa na Taasisi ya Viwango yanatokana na kodi kubwa zinazotozwa kwa wahusika jambo ambalo Kamati inahisi ni kuwaongezea watumiaji wa bidhaa mzigo hasa kwa bidhaa zinazotoka Tanzania Bara, kutokana na jambo hilo, Kamati inaishauri Taasisi ya Viwango kuhakikisha kuwa bidhaa zote zinazotoka Tanzania Bara zinakuwa na hati ya viwango ***(Certificate of conformity).***

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2021/2022 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imepanga kutekeleza Programu zake kuu nne kama ifuatavyo:

i) Programu ya Uendeshaji na uratibu wa Wizara ya Biashara;

ii) Programu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali;

iii) Programu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara; na

iv) Programu ya Viwango na Tathmini ya Ubora.

**Mheshimiwa Spika**, Katika utekelezaji wa Programu hizo, bajeti ya kutosha inahitajhika ili lengo liweze kufikiwa na wananchi waweze kunufaika. Pamoja na juhudi zilizochukuliwa na Serikali bado juhudi kubwa inahitajika kwa kuweka fedha za kutosha katika kila programu ili yale yalioahidiwa na Serikali yaweze kutimia. Kamati inasikitika sana kusema kuwa fedha zilizotengwa katika programu hizo hazitoshi kabisa kufikia kile kilichoahidiwa pamoja na kwamba ndio kwanza safari ya utekelezaji imeanza. Kamati bado inasisitiza uongezweaji wa bajeti katika programu zote pamoja na kupatika kwa wakati kwa fedha zilizotengwa ndani ya bajeti ili kile kidogo kinachotegemewa kufanyika kiweze kufanyika kwa mujibu wa mipango ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba sasa uniruhusu nieleze maoni ya Kamati katika kila programu ili tuweze kuona ni kwa kiasi gani tunaweza kufikia malengo ya kibajeti yaliyopangwa kwa mwaka huu.

## PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA BIASHARA

**Mheshimiwa Spika**, Programu hii utekelezaji wake unahitaji fedha za kutosha ili lengo liweze kufikiwa kutokana na mambo mengi ya msingi kubebwa katika programu hii. Mipango na mikakati yote ya Wizara inaingia katika programu hii pamoja na Ofisi kuu Pemba. Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii imesikitika sana kuona fedha zilizopangwa kwa mwaka huu wa fedha katika programu hii ni kidogo ukilinganisha na fedha za bajeti iliyopita. Ikumbukwe kwamba ili malengo yaweze kufikiwa tunahitaji fedha za kutosha kuyatimiza malengo hayo, hata hivyo inasikitisha kuona kuwa programu ambayo inabeba mambo mengi ya kimkakati haikupangiwa fedha za kutosha jambo ambalo lilipelekea Kamati kujiuliza jee tutaweza kutumiza yale yote yaliyoahidiwa na Serikali?

**Mheshimiwa Spika,** Ili Wizara iweze kuandaa na kuratibu majadiliano ya kibiashara ya kitaifa na kimataifa ambayo yatazaa tija kubwa kwa wafanya biashara wetu pamoja na kusimamia vyema takwimu za biashara na viwanda, fedha za kutosha zinahitajika. Kamati inayaeleza haya kutokana na hali halisi ilivyo sasa ambapo kwa bajeti iliyopita programu hii ilikadiriwa shilingi **3,526,977,000** ambapo fedha hizo hazikukidhi mahitaji kutokana na mafanikio kwa programu hii kutoridhisha. Kwa mwaka 2021/2022 programu hii imekadiriwa jumla ya shilingi **3,040,953,000** kwa ajili ya kutekeleza hayo ambayo nimeshaeleza hapo awali. Kamati inajiuliza ikiwa bajeti iliyopita malengo hayakufikiwa kikamilifu jee bajeti hii ambayo imepunguzwa ukilinganisha na bajeti iliyopita tutafikia hata nusu ya  mlengo? Tunaiomba Serikali ifanye tena mapitio katika vipaumbele kwa kila Wizara ili vile vipaumbele vinapopangwa na bajeti zake ziwe na uhalisia.

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kutoa pongeza kwa Serikali kwa juhudi zake inazoendelea kuzichukua katika suala zima la uimarishaji wa viwanda pamoja uimarishaji wa uzalishaji kwa wazalishaji wadogo wadogo. Programu hii kwa mwaka uliopita ilikadiriwa jumla ya shilingi **12,782,152,000** wakati kwa mwaka huu wa 2021/2022 programu hii imekadiriwa jumla ya shilingi **13,713,523,000**. Hata hivyo, pamoja na fedha kuongezeka katika programu hii, Kamati yangu inasisitiza umuhimu wa Idara ya Maendeleo ya Viwanda kuingiziwa fedha kwa mujibu wa bajeti ili Idara iweze kuwa na usimamizi mzuri wa kuviendeleza viwanda vinavyoanzishwa na wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,** kama tunavyofahamu kwamba kwa kiasi fulani hivi sasa wananchi wetu wamepata mwamko mkubwa wa kujikwamu na suala zima la umaskini jambo ambalo linawapelekea baadhi yao kujikusanya vikundi vidogo vidogo na kuanzisha viwanda vyao ambavyo wanavitegemea katika kuwaingizia kipato.

**Mheshimiwa Spika**, Miongoni mwa ahadi ambazo Mheshimiwa Rais alizizungumza katika hotuba yake ya ufunguzi wa Baraza hili, ni pamoja na kuielezea dhamira yake halisi kabisa ya kuhakikisha kwamba sekta binafsi inashiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mipango na mikakati iliyopo ya ujenzi wa viwanda vidogo vidogo, dhamira hii ya Mheshimiwa Rais haiwezi kufikiwa endapo Idara ya Maendeleo ya Viwanda haijawezeshwa kwa kuingiziwa fedha za kutosha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu baada ya kupitia bajeti ya programu hii, imeona kwamba suala la tathmini ya mazingira katika maeneo ya viwanda bado lina changamoto kubwa kutokana na kutengewa fedha kidogo. Kamati yangu inaamini kwamba ili tathmini na utekelezaji halisi uweze kufanyika katika suala hili fedha za kutosha zinahitajika ili wataalamu wetu waweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuishauri Serikali jinsi ya kufanya katika maeneo hayo ya viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu imebaini kwamba katika miradi ya maendeleo kwa maeneo ya Nungwi, Chamanangwe na Dunga hakuna kilichofanyika kutokana na fedha iliyotengwa ya utekelezaji wa miradi hiyo kutokidhi mahitaji. Kamati imebaini kwamba imekua ni jambo la kawaida kwetu sisi kutegemea sana bajeti za wafadhili katika utekelezaji wa miradi tujiyojipangia jambo ambalo sio sahihi kabisa. Kwa mnasaba huo, Kamati inaishauri Serikali kuitengea fedha za kutosha Idara ya Maendeleo ya Viwanda ili athari ya utekelezaji wa miradi inapofanyika iweze kuonekana kwa uwazi kabisa.

## PROGRAMU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA BIASHARA

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ya awamu ya nane ilieleza wazi azma yake ya kukuza sekta ya biashara kwa kushirikiana kikamilifu na sekta binafsi kwa lengo la kukuza kipato miongoni mwa wananchi wetu. Aidha, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya ufunguzi wa Baraza la Wawakilishi, alisema kuwa Serikali itahakikisha kuwa inavilinda viwanda vidogo vidogo na biashara zake kwa ujumla dhidi ya ushindani usio wa haki wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi ambazo hazilipiwi kodi stahiki.

**Mheshimiwa Spika**, azma hiyo ya Serikali kupitia bajeti ya mwaka huu tumeanza kuiona kupitia **Programu Ndogo ya "Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji"**, kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 programu hii imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi

**4,645,373,000** tofauti na bajeti ya mwaka 2020/2021 ambapo makadirio yalikua ni shilingi **856,301,000**. Kwa hatua hii Kamati inatoa pongezi sana na inaamini kwamba maendeleo endelevu kwa wafanyabiashara wetu yatapatikana.

**Mheshimiwa Spika**, Idara ya biashara na ukuzaji wa masoko katika utekelezaji wa majukumu yake, ni vyema ikaweka majukumu yake katika utaratibu mzuri ili yale malengo yaliyokusudiwa kutekelezwa yaweze kukamilika kwa wakati. Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii inaamini kwamba kwa mwaka wa 2021/2022 programu hii ambayo imepangiwa makadirio ya shilingi **13,790,024,000** itapiga hatua kubwa sana katika kukamilisha majukumu yake tofauti na mwaka wa 2020/2021 ambapo makadirio yalikuwa ni shilingi **3,316,771,000**.

**Mheshimiwa Spika,** tunaomba fedha zilizokadiriwa katika bajeti hii zipatikane kwa wakati na zipatikane kama zilivyokadiriwa.

## PROGRAMU YA VIWANGO NA TATHMINI YA UBORA

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii ni miongoni mwa programu ambazo kwa mwaka ujao wa fedha zimechamnganywa na programu nyengine ili kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa kufanyika katika kipindi kifupi. Progamu hii imechanganywa na Programu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara na ndio maana fedha za program hiyo zimepanda kwa kiasi kikubwa. Kama nilivyotoa maelezo katika progamu ya juu kuwa tuna matumaini makubwa kuwa katika utekelezaji wa bajeti hii, endapo fedha zilizotengwa zitaingizwa na kupatikana kwa wakati, athari ya kiutendaji na utekelezaji wa program hizo itaonekana wazi wazi.

**Mheshimiwa Spika,** tunamini kuwa suala la vikwazo vya kibiashara ambalo kwa sasa imekuwa ni changamoto kubwa kabisa kwa wafanyabiashara wetu wa Zanzibar, likifanyiwa kazi na kuwekwa sawa kwa kuangaliwa viwango na ubora wa bidhaa kutoka Zanzibar, tunaamini kuwa wafanyabiashara wetu watafanya vizuri sana katika soko la ndanii na nje ya nchi endapo wakijengewa mazingira mazuri ya biashara.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Kamati yangu iliipitia bajeti ya Wizara hii na baada ya kutoa miongozo na maelekezo mbali mbali kwa Wizara na kukubaliana kuyatekeleza maelekezo hayo, tuliridhika na bajeti na tunaamini kuwa kutokana na umakini wa Mheshimiwa Waziri na watendaji wa Wizara hii,utekelezaji wake utakua na ufanisi mkubwa. Pamoja na hayo, bado Kamati inasisitiza kuwa kwa Idara na Taasisi zote za Wizara hii ambazo mfumo wa ukusanyaji wa mapato unatumia mfumo maalum **'system'** tunapendekeza kuwa kwa idara hizo zitoe elimu juu ya jambo hilo kwa jamii ili wananchi wapate uelewa zaidi kuhusiana na jambo hilo pamoja na kuondoa masuali

kwa Waheshimiwa Wajumbe ambao baadhi yao walikua na masuali mengi kuhusiana na mapato ya baadhi ya taasisi za Pemba ambazo hawakuona mapato yake yanakwenda wapi.

**Mheshimiwa Spika**, kupitia Programu ndogo ya Viwango na Udhibiti wa Ubora tunaiomba Serikali kufanya juhudi za makusudi kuzuia ongezeko la mfumuko wa bei hasa kwa wananchi wa kisiwa cha Pemba. Kamati imeamua kulizungumzia hili kutokana na ukweli kwamba bei za bidhaa nyingi za vyakula ziko juu kisiwani Pemba ukilinganisha na Unguja, hali ambayo inapelekea ongezeko la ugumu wa maisha kwa wananchi wa kisiwa hicho.

**Mheshimiwa Spika**, Unguja na Pemba ni nchi moja lakini hali ya kuongezeka kwa bei za bidhaa mara kwa mara linatupa mashaka na kusababasha wananchi walio wengi wa kisiwa cha Pemba kukosa imani na Serikali yao.

## SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC)

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Biashara la Taifa lina wajibu wa kuhakikisha kuwa wananchi wa visiwa hivi wananufaika na mazao ya biashara wanayozalisha, aidha, Shirika lina jukumu kubwa la kununua na kuuza karafuu na mazao mengine ya kilimo kwa lengo kunyanyua kipato cha wananchi na kuimarisha uchumi wa taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa miaka ya hivi karibuni, zao la karafuu lilipandishwa sana bei kwa hapa kwetu na wananchi wanaojihusisha na ukulima wa zao hilo ,wamekua wakipata faida kubwa kupitia mauzo ya karafuu. Hata hivyo, pamoja na upandishaji huo wa bei, Shirika limekua likinunua zao hilo kutoka wananchi kwa hasara kubwa sana jambo ambalo limepelekea Shirika letu kuwa na madeni mengi na kujiendesha kwa hasara kubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipewa tarifa kuwa kwa sasa Shirika linadaiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) shilingi Bilioni 5, Benki ya watu wa Zanzibar (PBZ) shilingi Bilioni 8, wateja wa karafuu wanalidai Shirika shilingi Bilioni 6.7, Shirika la umeme (ZECO) Milioni 7 na kampuni ya Selem Construction wanalidai Shirika shilingi milioni 1.1 pamoja na wafanyakazi wa Shirika waliostaafu ambao wapo 225 wanalidai Shirika shilingi Bilioni 22 hadi wakati Kamati inafika katika Shirika hilo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipofanya ziara katika Shirika hili ilibaini changamoto nyingi ambazo utatuzi wake unahitaji fedha nyingi sana zitakazolinusuru Shirika hilo lisiweze kufilisika. Aidha tunachukua nafasi hii pamoja na changamoto nyingi zilizopo kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kushuka kwa wananchi na kuwaeleza hali

halisi kuhusiana na bei ya karafuu na baada ya kutoa maelezo hayo, Serikali imeamua kuishusha bei hiyo ili iendane na soko la dunia na hatimae kulinususru Shirika hilo.

**Mheshimiwa Spika**, ili Shirika liweze kujiendesha na kusimama lenyewe bila kuyumba linahitaji kujitathmini kwa kuanza kufikiria upya miradi mbali mbali iliyoanzishwa na Shirika kwa kuviimarisha vitega uchumi vyake pamoja na kurudi katika majukumu yake ya asili kama yaliyvyoelezwa na sheria iliyoanzisha Shirika hili.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inasisitiza kuimarishwa kwa Shirika hili kutokana na ukweli kwamba kuna baadhi ya wafanyakazi ni wa ajira za mkataba. Jambo hilo linarudisha nyuma maendeleo ya Shirika wakiwemo wafanyakazi waliopo Saateni ambao Kamati inaona kuwa ni vyema wakaajiriwa ili kuongeza nguvu kazi ya taifa. Aidha, Kamati inasisitiza umuhimu wa kumaliza matenegenzo na marekebisho yaliyokua yakifanywa katika kiwanda cha Makonyo Pemba kwa kumsisitiza mkandarasi aliyekuwa akifanya matengenezo hayo kurudi na kumalizakazi yake ili kiwanda kiweze kuzalisha na kuleta tija.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho naomba nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii katika Baraza lako tukufu, pia niwashukuru Wajumbe wako kwa utulivu wao waliouonesha wakati nawasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** Nawaomba Wajumbe wako waichangie bajeti hii, wahoji na watoe mapendekezo yao ili tuweze kuipitisha baada ya kuafikiana kwa hoja mbali mbali watakazoziibua wakati wa mjadala.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

…………………………………….

**Azza Januari Joseph,**

**Makamo Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii,**

**Baraza la Wawakilishi,**

**<u>Zanzibar.</u>**